# Mbele ya malaika

## Siku ya Mungu ya tano katika mwaka C

Composit: Yanick NGOY MWILAMBWE

Pas vite

Zaburi 137, 1-2a, 2bc-3, 4-5, 7c-8




1. Nitakutukuza, Ee Bwana, kwa moyo wangu wo**te**
   kwani umesikia maneno ya kinywa **changu**
   mbele ya malaika nitakui**mbia**
   nitaliangukiya hekalu lako **ta**katifu

2. Nitatukuza jina la**ko**
   kwa ajili ya wema na uaminifu **wako**
   siku nilipo kuita ulinisiki**liza**
   uliongeza nguvu ro**ho**ni mwangu

3. Wafalme wote wa dunia, watakutukuza Ee Bwa**na**
   watakapo sikia maneno ya kinywa **chako**
   wataziimba njiya ya **Bwana**
   kweli, utukufu wa Bwa**na** ni mkubwa

4. Mkono wako wakuume unanisalimi**sha**
   Bwana atatimiliza kwangu aliyonite**ndea**
   Ee Bwana, wema wako ndio wa mi**lele**
   usiache kazi ya mi**ko**no yako